

# Musaada Toka Juu

KIMETUNGWA
NA WATSON GOODMAN

GRATUIT — PASIPO BEI

# MUSAADA TOKA JUU

**"MUSAADA TOKA JUU" ni kitabu kinachokutanisha maandiko fulani ya Biblia juu ya maneno makubwa yanayofundishwa katika Biblia. Ninaamini ya kama maana ya Maandiko inajulikana kwa kupambanisha maandiko ya Biblia.**

**Neno la Mungu linatoka "juu" na ni musaada kwa wale wanaokuwa na hamu sana ya kufuata mambo yaliyo haki. Wakati mutu anapogeuza nia yake mbaya kwa kukataa zambi na kumupokea Bwana Yesu Kristo kuwa mwokozi wake, Mungu anamupa furaha na amani moyoni mwake. Katika mwaka wa 1937 mimi nilipata kumujua Bwana na hata leo ninaendelea kushirikiana Naye. Ikiwa wewe bado kumukubali Bwana Yesu Kristo, ninakusihi kujitoa kwake Bwana SASA kusudi apate kuwa Mwokozi wako na Bwana wako. —Watson Goodman (1920-2002)**

Yeremia 31:3

BWANA alinitokea zamani akisema: Ndiyo, nimekupenda kwa mapendo ya milele, kwa sababu hii nimekuvuta kwa wema wa mapendo yangu.

Yoane 15:13

Hakuna mwenye mapendo kuliko haya, mutu kutoa uzima wake kwa sababu ya rafiki zake.

Waroma 5:8

Lakini Mungu anaonyesha mapendo yake kwetu, wakati tulipokuwa tungali wenye zambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.

Na zinazotoka kwa Yesu Kristo, mushuhuda aliye mwaminifu, muzaliwa wa kwanza wao waliokufa, na mukubwa wa wafalme wa dunia. Kwake yeye aliyetupenda na kutuosha zambi zetu kwa damu yake. — Ufunuo 1:5

Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili kila mutu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele. — Yoane 3:16

Yoane 13:1

Basi mbele ya karamu ya Pasaka, Yesu akijua saa yake imefika aondoke dunia hii kwenda kwa Baba, akiwa amependa watu wake waliokuwa katika dunia, aliwapenda hata mwisho.

**Matayo 1:22, 23**

Maneno haya yote yamekuwa ili litimie neno lililosemwa na Bwana kwa nabii, akisema: Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana, Nao watamwita jina lake Emanueli; maana yake Mungu pamoja nasi.

**Yoane 14:9, 10a**

Yesu akamwambia: Nimekuwa pamoja nanyi wakati murefu na hukunijua, Filipo? Aliyeniona mimi, ameona Baba; namna gani unasema: Utuonyeshe Baba? Huamini ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani yangu?

**1 Timoteo 3:16**

Na pasipo shaka, siri ya utawa ni kubwa: Mungu alionekana katika mwili, Alihesabiwa kuwa na haki katika Roho, Alionekana na malaika, Alihubiriwa katika mataifa, Aliaminiwa katika ulimwengu, Alipokewa katika utukufu.

**Yoane 1:1, 14**

Katika mwanzo alikuwa Neno, na Neno alikuwa pamoja na Mungu, na Neno alikuwa Mungu. . . . Na Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, tukatazama utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee akitoka kwa Baba, amejaa neema na kweli.

### Wakolosayi 2:9

Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa mwili.

### Matayo 17:5

Wakati alipokuwa akisema, tazama wingu la kungaa likawafunga kwa kivuli; na tazama, sauti toka wingu ikisema: Huyu ni Mwana wangu, mupendwa wangu, ninayependezwa naye; sikieni yeye.

### Isaya 9:6

Maana kwa ajili yetu mutoto amezaliwa, Tumepewa mutoto mwanamume; Na utawala utakuwa juu ya bega lake: Na jina lake litaitwa Mwenye ajabu, Mwenye shauri, Mungu Mwenye uwezo, Baba ya milele, Mukubwa wa salama.

### 1 Yoane 4:15

Kila mutu anayekiri ya kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, Mungu anakaa ndani yake naye ndani ya Mungu.

### Luka 1:35

Malaika akamujibu akamwambia: Roho Mutakatifu atakuja juu yako, na nguvu zake Mungu aliye juu zitakutulia kivuli; kwani kile kitu kitakachozaliwa nawe kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu.

Nikingali katika dunia, mimi ni nuru ya dunia. —Yoane 9:5

Basi Yesu aliwaambia tena: Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Mimi ni mulango wa kondoo.
—Yoane 10:7

Yesu akawaambia: Mimi ni mukate wa uzima, yeye anayekuja kwangu hatasikia njaa kabisa, naye mwenye kuniamini hataona kiu kabisa. —Yoane 6:35

Yule mwanamuke akamwambia: Ninajua Masiya anakuja (anayeitwa Kristo): kama yeye atakapokuja, atatuambia maneno yote. Yesu akamwambia: Mimi ninayesema nawe, ndiye.
—Yoane 4:25, 26

Yesu akamwambia: Mimi ni ufufuko na uzima: yeye anayeniamini, hata anapokufa, ataishi.
—Yoane 11:25

Munaniita Mwalimu na Bwana: na munasema vema, sababu nilivyo hivi. —Yoane 13:13

Akawaambia: Munatoka chini, ninatoka juu; ninyi ni wa dunia hii, mimi si wa dunia hii.
—Yoane 8:23

Yesu akawaambia: Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Mbele Abrahamu hajazaliwa, mimi niko.
—Yoane 8:58

### Matayo 20:30, 34

Na tazama, vipofu wawili walikuwa wakiketi kando ya njia, na wakati waliposikia ya kwamba Yesu anapita, walipaza sauti wakisema: Bwana, uturehemu, wewe Mwana wa Daudi . . . Yesu akawahurumia, akagusa macho yao; mara moja wakapata kuona, wakamufuata.

### Luka 5:4-6

Alipokwisha kusema, akamwambia Simoni: Mwende sasa kilindini, mukashushe mikila yenu kwa uvuvi. Simoni akajibu akamwambia: Bwana, tumefanya kazi kwa nguvu usiku kucha wala hatukupata kitu: lakini kwa neno lako nitashusha mikila. Na wakati walipofanya hivi, walipata samaki wengi sana hata mikila yao ikaanza kukatika.

### Matayo 14:19-21

Akaamuru makutano kuketi katika majani; akatwaa mikate mitano na samaki mbili, na akitazama mbinguni akabariki, akavunja na kuwapa wanafunzi mikate, wanafunzi wakawapa makutano. Nao wote wakakula, wakashiba; wakaokota vya vipande vilivyobaki vitunga kumi na viwili. Nao waliokula walikuwa waume kama elfu tano, pamoja na wanawake na watoto.

Waroma 14:9

Kwa sababu hii Kristo alikufa, na alifufuka awe Bwana yao waliokufa, nao walio hai vilevile.

Waebrania 1:2

Mungu . . . katika siku hizi za mwisho amesema nasi katika Mwana, aliyemuweka kuwa muriti wa vitu vyote, kwa yeye aliyefanya ulimwengu.

Wakolosayi 1:16

Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa vilivyo mbinguni na vilivyo duniani, vitu vinavyoonekana na visivyoonekana, ikiwa ni viti vya wafalme ao usultani ao falme ao mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake na kwa ajili yake.

Yoane 1:3

Vitu vyote vilifanyika kwa huyu; na pasipo yeye hakikufanyika hata kitu kimoja kilichofanyika.

1 Wakorinto 1:9

Mungu ni mwaminifu muliyeitwa naye katika ushirika wa Mwana wake Yesu Kristo Bwana wetu.

Matendo 2:36

Basi kila nyumba yote ya Israeli ijue kwa kweli, Mungu amefanya huyu Yesu muliyemusulibisha kuwa Bwana na Kristo.

**Matayo 25:32**
Na mbele yake mataifa yote watakusanyika; naye atawatenga kama muchungaji anavyotenga kondoo na mbuzi.

**Yoane 5:22**
Maana Baba hamuhukumu, hata mutu mumoja, lakini amemupa Mwana hukumu yote.

**Waroma 14:10**
Lakini wewe, kwa nini unahukumu ndugu yako? na wewe, kwa nini unazarau ndugu yako? Kwa sababu sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

**Waroma 2:16**
Katika siku ile Mungu atakapohukumu siri za watu, sawasawa na Habari Njema yangu, kwa Yesu Kristo.

**2 Timoteo 4:1**
Ninakuagiza mbele ya Mungu, na ya Bwana Yesu Kristo, atakayewahukumu walio hai na waliokufa, na kwa kuonekana kwake, na kwa ufalme wake.

**Matendo 10:42**
Akatuagiza tuhubiri watu, na kushuhudu ya kuwa ndiye yeye aliyeamriwa na Mungu awe Mwamuzi wa wahai na wafu.

**Matendo 4:12**
Wala hakuna wokovu katika mwingine, kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu waliopewa watu tupate kuokolewa nalo.

**Waebrania 7:25**
Naye, kwa sababu hii anaweza kuokoa kabisa wao wanaokuja kwake Mungu kwa njia yake; maana yeye ni hai siku zote apate kuwaombea.

**Yoane 10:9**
Mimi ni mulango; kama mutu ataingia kwa mimi, atakolewa, na ataingia na kutoka, naye atapata chakula.

**Yoane 14:6**
Yesu akamwambia: Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima: mutu hakuji kwa Baba, ila kwa mimi.

**Yoane 8:24**
Basi niliwaambia ninyi: Mutakufa katika zambi zenu; kwa sababu musipoamini ya kama mimi ndiye, mutakufa katika zambi zenu.

**Waebrania 5:9**
Naye alipokwisha kukamilishwa, akakuwa mutengenezaji wa wokovu wa milele kwa watu wote wenye kumutii.

Waroma 3:24

Wanahesabiwa haki bule kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Yesu Kristo.

Luka 19:10

Maana Mwana wa watu alikuja kutafuta na kuokoa yule aliyepotea.

1 Wakorinto 1:30

Lakini kwa yeye ninyi ni katika Yesu, aliyefanyizwa na Mungu kuwa kwetu akili, na haki, na utakaso na ukombozi.

Ufunuo 5:9

Nao wanaimba wimbo mupya, wakisema: Umestahili wewe kutwaa kitabu na kufungua mihuri yake; kwa sababu ulichinjwa, ukanunulia Mungu kwa damu yako, watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa.

Tito 2:14

Aliyejitoa mwenyewe kwa ajili yetu atukomboe toka uovu wote, na kujisafishia watu wawe mali yake mwenyewe, wenye bidii sana katika kazi njema.

Wakolosayi 1:12-14

Mukishukuru Baba aliyetustahilisha kupokea sehemu ya uriti wa watakaifu katka nuru. Naye alitutoa katika uwezo wa giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa mapendo yake; ndani yake tuna wokovu wetu, usamehe wa zambi zetu.

### Waefeso 1:7

Katika yeye tuna ukombozi wetu kwa njia ya damu yake, usamehe wa zambi zetu, sawasawa na wingi wa neema yake.

### 1 Yoane 1:7

Lakini kama tukitembea katika nuru, kama yeye alivyo katika nuru, tunashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, inatusafisha zambi zote.

### 1 Petro 1:18, 19

Mukijua mumekombolewa, si kwa vitu vinavyoharibika, kwa feza ao zahabu, mupate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa muliopokea kwa baba zenu; lakini kwa damu ya damani, kama ya kondoo asiye na kilema wala alama, damu ya Kristo.

### Waebrania 9:14

Basi si zaidi damu ya Kristo, ndiye kwa Roho ya milele, alijitoa mwenyewe kwa Mungu, kuwa zabihu isiyo na alama, itasafisha zamiri zenu na matendo ya kufa, mupate kutumikia Mungu aliye hai?

### Waroma 5:9

Basi zaidi sana tukihesabiwa haki sasa kwa damu yake, tutaokolewa katika gazabu kwa yeye.

### Wagalatia 5:6

Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa; lakini imani inayotenda kazi kwa mapendo.

### Waroma 5:1

Basi tukikwisha kuhesabiwa haki kwa njia ya imani, tuna salama kwa Mungu kwa njia ya Bwana yetu Yesu Kristo.

### Waefeso 2:8, 9

Kwa maana mumeokolewa kwa neema kwa njia ya imani, wala neno hili halikutoka ndani yenu wenyewe, ni zawadi ya Mungu, si kwa matendo, asiwe mutu atakayejisifu.

### Yoane 20:31

Lakini hizi zimeandikwa mupate kuamini ya kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mupate uzima kwa jina lake.

### 1 Yoane 5:4

Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu kinashinda dunia; na hii ni kushinda kunakoshinda dunia, imani yetu.

### Yoane 6:28, 29

Halafu walimwambia: Tufanye nini, tupate kufanya kazi za Mungu? Yesu akajibu, akawaambia: Hii ni kazi ya Mungu, mumwamini yeye aliyetumwa naye.

### Zaburi 108:4

Maana rehema yako ni kubwa juu ya mbingu, Na kweli yako hata mawinguni.

### Zaburi 103:11

Maana sawasawa mbingu zilivyo juu sana kupita inchi, Kwa kadiri ile rehema yake ni kwao wanaomwogopa.

### Zaburi 103:17

Lakini wema wa BWANA ni tangu milele hata milele juu yao wanaomwogopa, Na haki yake kwa wana wa wana.

### Maombolezo 3:22, 23

Ni kwa sababu ya rehema za BWANA hatuangamizwi, kwa sababu huruma zake hazikomi. Ni mpya kila asubui; uaminifu wako ni mukubwa.

### Tito 3:5

Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyafanya, lakini kwa rehema yake alituokoa, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa mupya na kufanywa upya na Roho Mutakatifu.

### Mika 7:18

Nani ni Mungu kama wewe, anayesamehe uovu, na anayepita juu ya kosa la baki la uriti wake? Hachungi kasirani yake kwa milele, kwa maana anapendezwa na rehema.

**Ufunuo 22:17**

Na Roho na bibi-arusi wanasema: Kuja. Naye mwenye kusikia aseme: Kuja. Naye mwenye kiu, aje; na yeye anayetaka atwae maji ya uzima bule.

**Yoane 7:37**

Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya karamu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake, akisema: Mutu akiona kiu aje kwangu, anywe.

**Isaya 55:1**

Haya, kila mutu anayeona kiu, muje kwa maji, Naye asiye na feza; muje, mununue na mule; Ndiyo, muje, mununue mvinyo na maziwa, Pasipo feza na pasipo bei!

**Matayo 11:28**

Kujeni kwangu, ninyi wote munaosumbuka na wenye muzigo muzito, nami nitawapumzisha ninyi.

**Isaya 1:18**

Haya, kujeni, na tufanye shauri pamoja, BWANA anasema, hata zambi zenu ni nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kabisa kama theluji: hata ni nyekundu kama nyekundu ya damu zitakuwa kama manyoya ya kondoo.

Lakini wote waliomupokea aliwapa uwezo wa kuwa watoto wa Mungu, ndio wale walioamini jina lake. — Yoane 1:12

Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho ya Mungu, hawa ndio wana wa Mungu. Kwa maana hamukupokea tena roho ya utumwa inayoleta woga, lakini mulipokea roho ya kufanywa wana, kwa sababu hii tunalia: Aba, Baba. — Waroma 8:14, 15

Mupate kuwa wana wa Mungu wasio na laumu wala udanganyifu, pasipo kipaku katika kizazi cha jeuri na ubishi, katikati yao ninyi munaonekana kama taa katika ulimwengu. —Wafilipi 2:15

Kwa sababu ya neno hili, Tokeni kaikati yao, mukatengwa nao, Bwana anasema, Wala musiguse kitu kisicho safi; Nami nitawapokea ninyi, Nitakuwa baba kwenu, Nanyi mutakuwa kwangu wana na binti, Bwana Mwenyezi anasema.

—2 Wakorinto 6:17, 18

Hivi watoto wa Mungu wanaonekana wazi, na watoto wa Shetani; mutu ye yote asiyetenda haki hatoki kwa Mungu, wala yeye asiyependa ndugu yake.

—1 Yoane 3:10

### Mezali 23:31, 32

Wewe usiangalie mvinyo wakati ilipo nyekundu, Wakati inapotoa rangi yake ndani ya kikombe, Wakati inaposhuka pasipo matata. Kwa mwisho inauma kama nyoka, Na kuchoma kama fira.

### Wagalatia 5:19-21

Basi matendo ya mwili yanaonekana, ndiyo: uasherati, uchafu, uzini, kuabudu sanamu, ulozi, uadui, ugomvi, uwivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, uuaji wa mutu, ulevi, ulafi, na yanayofanana na maneno haya; juu ya maneno haya ninawaambia ninyi mbele kama nilivyowaambia ninyi zamani; watu wale wanaotenda maneno ya namna hii, hawatariti ufalme wa Mungu.

### Isaya 5:11

Ole wao wanaoamka asubui mapema, wafuate ulevi; wale wanaoshinda hata usiku, mupaka mvinyo inawaka kama moto ndani yao!

### Waroma 13:13, 14

Kama katika muchana, tutembee vizuri; si kwa ulafi na ulevi, si kwa uasherati na tamaa mbaya, si kwa kugombana na wivu. Lakini muvae Bwana Yesu Kristo, na musifikili mahitaji ya mwili, kutimiza tamaa zake.

Matayo 22:37, 38

Akamwambia: Upende Bwana Mungu wako na moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ni amri iliyo kubwa na ya kwanza.

Marko 10:17-22

Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mutu mumoja akakuja mbio, akapiga magoti mbele yake, akamwuliza: Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuriti uzima wa milele? Yesu akamwambia: Kwa nini unaniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mumoja, ndiye Mungu. Unajua amri: Usiue, usizini, usiibe, usishuhudie uwongo, usidanganye, uheshimu baba yako na mama yako. Akamwambia: Mwalimu, nimetii maneno haya yote tangu utoto wangu. Yesu akamutazama, akamupenda, akamwambia: Umepungukiwa na neno moja: kwenda zako, ukauze vitu ulivyo navyo, uwape masikini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha unifuate. Lakini alikunja uso kwa neno hili, akakwenda zake kwa huzuni, kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

Mezali 16:25

Kuna njia inayoonekana kuwa sawa kwa macho ya mutu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti.

Maana mutu akijizania kuwa kitu, naye si kitu, anajidanganya yeye mwenyewe. —Wagalatia 6:3

Lakini muwe watenda wa neno, wala si wasikiaji tu, mukijidanganya wenyewe.
—Yakobo 1:22

Mutu asiwadanganye ninyi na maneno bule; kwa kuwa kwa sababu ya maneno haya kasirani ya Mungu inakuja juu ya wana wa kuasi. —Waefeso 5:6

Watoto wadogo mutu asiwadanganye ninyi; yeye anayetenda haki, ndiye ana haki, kama yeye alivyo na haki. Yeye anayetenda zambi ni wa Shetani; kwa kuwa Shetani anatenda zambi tangu mwanzo. . . . —1 Yoane 3:7, 8a

Musidanganywe: Mungu hazihakiwi; yo yote mutu anayopanda, ndiyo atakayovuna.
—Wagalatia 6:7

Hamujui ya kama wazalimu hawatariti ufalme wa Mungu? Musidanganywe: waasherati, wala wenye kuabudu sanamu, wala wazini, wala wakike wala wafiraji, wala wizi, wala wenye tamaa, wala walevi, wala watukanaji wala wanyanganyi hawatariti ufalme wa Mungu.
—1 Wakorinto 6:9, 10

Yakobo 1:15

Halafu tamaa ikizaa, inazaa zambi na ile zambi ikikwisha kukomea, inazaa mauti.

Waroma 5:12

Hivi, kama kwa mutu mumoja zambi iliingia ulimwenguni, na kufa kwa njia ya zambi; na hivi kufa kulikuja juu ya watu wote, kwa sababu wote wamefanya zambi.

Waroma 8:6, 7

Kwa maana nia ya mwili ni kufa; lakini nia ya Roho ni uzima na salama: kwa sababu nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi.

Ezekieli 18:20

Nafsi inayofanya zambi itakufa, mwana hatabeba uovu wa baba, wala baba hatabeba uovu wa mwana; haki ya mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wa mwovu utakuwa juu yake.

Luka 15:32

Ilitufaa kufurahi na kuchekelea, kwa maana huyu ndugu yako alikufa, naye ameishi tena; alipotea, naye ameonekana.

Mezali 11:19

Mwenye kudumu katika haki atapata uzima: Lakini mwenye kufuata uovu anaufuata kwa mauti yake mwenyewe.

### Yoane 10:17, 18

Hivi Baba ananipenda, kwa sababu ninatoa uzima wangu, ili niutwae tena. Hakuna mutu anayeuondoa kwangu, lakini mimi mwenyewe ninautoa. Nina uwezo kuutoa, na nina uwezo kuutwaa tena. Agizo hili nililipokea kwa Baba yangu.

### 1 Wakorinto 15:3, 4

Kwa sababu kwanza niliwapasha ninyi habari za maneno niliyopokea vilevile: ya kwamba Kristo alikufa kwa sababu ya zambi zetu kama maandiko yanavyosema; na ya kama alizikwa, akafufuka siku ya tatu, kama maandiko yanavyosema.

### Ufunuo 1:18

Na aliye hai; nami nilikuwa nimekufa, na tazama, mimi ni hai hata milele na milele. Nami nina funguo za mauti, na za Hadeze.

### Yoane 11:43, 44

Wakati alipokwisha kusema maneno haya, akapaza sauti kubwa: Lazaro, toka inje. Na yule aliyekufa akatoka inje, akifungwa mikono na miguu kwa sanda, na uso wake umefungwa kwa kitambaa. Yesu akawaambia: Mumufungue, aende zake.

Kumbukumbu la Torati 5:7-21

Usiwe na miungu mingine ila mimi.

Usijifanyie sanamu ya kuchonga, mufano wa kitu cho chote juu mbinguni ao chini duniani, ao ndani ya maji chini ya inchi; usijiiname mbele yao wala kuzitumikia . . .

Usitaje jina la BWANA Mungu wako bule: maana BWANA hatamuhesabu kuwa hana kosa mutu anayetaja jina lake bule.

Shika sabato na kuitakasa, kama BWANA Mungu wako alivyokuamuru. Siku sita utatumika na kufanya kazi yako yote: lakini siku ya saba ni sabato kwa BWANA Mungu wako . . .

Heshimu baba yako na mama yako, kama BWANA Mungu wako alivyokuamuru . . .

Usiue.

Wala usizini.

Wala usiibe.

Wala usishuhudie jirani yako uwongo.

Usitamani muke wa jirani yako; wala usitamani nyumba ya jirani yako, wala shamba lake, wala mutumishi wake, wala kijakazi chake, ngombe ndume yake wala punda yake, wala kitu cho chote kilicho cha jirani yako.

Yobu 34:21, 22

Maana macho yake ni juu ya njia za mutu, Na anaona miendo yake yote. Hakuna giza, wala kivuli cha mauti, Pahali watenda uovu wanapoweza kujificha.

Yeremia 23:24

Mutu ye yote anaweza kujificha pahali pa siri, nisimwone? anasema BWANA. Si mimi ninayejaza mbingu na inchi? anasema BWANA.

Zaburi 139:8, 12

Nikipanda mbinguni, wewe ni kule: Nikifanya kitanda changu katika Hadeze, tazama, wewe ni kule . . . Hata giza halikufichii kitu, Lakini usiku unangaa kama muchana: Giza na nuru kwako ni sawasawa.

Mezali 15:3

Macho ya BWANA ni katika kila pahali, Yakitzama wabaya na walio wema.

Waebrania 4:13

Hakuna kiumbe kinachofichwa mbele yake, lakini vitu vyote ni utupu na kufunuliwa mbele ya macho yake yeye aliye na maneno yetu.

Luka 8:17

Kwa maana hakuna neno lililowekwa kwa siri lisiloonekana, wala neno lililofichwa, ila litafunuliwa na kuonekana wazi.

Na ikiwa mutu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.
—Ufunuo 20:15

Lakini mbingu zilizo sasa, na dunia, zimewekwa akiba kwa moto kwa neno hili, zikilindwa hata siku ya hukumu na uharibifu wao wasioogopa Mungu.
—2 Petero 3:7

Waovu watarudi kwa Hadeze,
Hata mataifa yote wanaosahau Mungu. —Zaburi 9:17

Kama mukono wako, ao muguu wako ukikukosesha, uukate na kuutupa mbali nawe; ni afazali kuingia katika uzima mwenye kilema na kiwete kuliko kuwa na mikono miwili ao miguu miwili kutupwa katika moto wa milele.
—Matayo 18:8

Mwana wa watu atatuma malaika zake, nao wataokota toka ufalme wake vitu vyote vinavyokwaza, nao wanaotenda uovu, na kuwatupa katika tanuru ya moto; kule kutakuwa kulia na kusaga meno. —Matayo 13:41, 42

Na hawa wote watakwenda kuingia katika azabu ya milele; lakini wenye haki watakwenda kuingia katika uzima wa milele.
—Matayo 25:46

**2 Petro 2:9**

Basi Bwana anajua namna gani kuokoa watawa katika majaribu na kuweka wasio haki katika hali ya azabu hata siku ya hukumu.

**Waebrania 9:27**

Na sawasawa watu wanavyowekwa kufa mara moja, na nyuma ya kufa hukumu.

**Matendo 17:31**

Kwa maana ameweka siku, atakayohukumu dunia kwa haki, kwa mutu yule aliyemuweka kwa kazi hii, naye aliwapa watu wote hakika ya mambo haya kwa kumufufua toka wafu.

**Waroma 14:12**

Basi kwa hii kila mumoja wetu atatoa habari zake mwenyewe mbele ya Mungu.

**1 Yoane 4:17**

Hivi mapendo yamekamilishwa kwetu, ili tuwe na uhodari katika siku ya hukumu; kwa sababu kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo sisi katika ulimwengu huu.

**2 Wakorinto 5:10**

Kwa sababu imetupasa sisi sote kuonekana mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo; hata kila mutu apokee maneno aliyotenda kwa mwili, kwa kadiri alivyotenda, kama ni mazuri ao mabaya.

1 Petro 5:5b

...kwa sababu Mungu anashindana na wenye kiburi, lakini anawapa wanyenyekevu neema.

2 Wakorinto 8:9

Kwa maana munajua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, namna alivyokuwa tajiri, lakini kwa ajili yenu alikuwa masikini, hata ninyi mupate kuwa matajiri kwa umasikini wake

Waroma 5:15

Lakini zawadi ya neema haikuwa kama lile kosa. Kwa maana kwa kosa la mutu mumoja wengi walikufa, zaidi sana neema ya Mungu, na zawadi kwa njia ya neema ya mutu mumoja, Yesu Kristo, imezidi kwa watu wengi.

Matendo 4:33

Na mitume walishuhudia ufufuko wake Bwana Yesu kwa nguvu nyingi. Neema kubwa ikakuwa juu yao wote.

Waroma 9:16

Basi, kama ni hivyo, si katika uwezo wa mwenye kutaka wala mwenye kupiga mbio, lakini wa Mungu anayerehemu.

2 Wakorinto 9:15

Mungu ashukuriwe kwa sababu ya zawadi yake tusiyoweza kuisifu kama inavyopasa.

**Matendo 3:19**

Tubuni basi, mugeuke, ili zambi zenu ziondoshwe, zipate kuja nyakati za ufufuko toka uso wa Bwana.

**Matendo 17:30**

Wakati huu wa ujinga Mungu hakuangalia, lakini sasa, ameamuru watu wote pahali po pote watubu.

**Luka 13:3**

Ninawaambia ninyi, Sivyo, lakini musipotubu, mutaangamia wote, sawasawa nao.

**Matendo 2:38**

Petro akawaambia: Tubuni mukabatizwe kila mumoja kwa jina lake Yesu Kristo, mupate ondoleo la zambi zenu, nanyi mutapokea zawadi ya Roho Mutakatifu.

**2 Wakorinto 7:10**

Kwa sababu huzuni iliyo mbele ya Mungu inafanyiza toba inayoleta wokovu, isiyo na majuto; lakini huzuni ya dunia inafanyiza mauti.

**Mezali 28:13**

Yeye anayefunika makosa yake hatasitawi: Lakini yeye anayeyakiri na kuyaacha atapata rehema.

**Matayo 3:2**

Akisema: Tubuni, sababu ufalme wa mbinguni umekaribia.

Tazama, ninasimama kwa mulango, ninapiga hodi; kama mutu akisikia sauti yangu na kufungua mulango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami. — Ufunuo 3:20

Matayo 6:14

Kwa sababu kama ninyi munasamehe watu makosa yao, Baba yenu ya mbinguni atawasamehe ninyi vilevile.

Ezekieli 18:21

Lakini kama mwovu akigeuka toka zambi zake zote alizozitenda, na kuchunga sheria zangu zote, na kutenda hukumu na haki, hakika ataishi, hatakufa.

Marko 2:5

Yesu akiona imani yao alisema kwa mutu mwenye kupooza: Mwana, zambi zako zinasamehewa.

Isaya 55:7

Mutu mubaya aache njia yake, Na mutu asiye haki aache mafikili yake; Na arudi kwa BWANA, Naye atamurehemu; Na kwa Mungu wetu, Naye atamusamehe kabisa kabisa.

Matendo 5:31

Mutu huyu Mungu amemutukuza kwa mukono wake wa kuume, apate kuwa Mukubwa na Mwokozi, ili awape Waisraeli toba na usamehe wa zambi.

Isaya 1:16

Mujioshe, mujitakase; mwondoshe uovu wa matendo yenu toka mbele ya macho yangu; mwache kufanya uovu.

Waefeso 5:11

Wala musishirikiane na matendo ya giza yasiyozaa matunda, lakini zaidi muyahamakie.

Wakolosayi 3:2

Tieni mafikili yenu juu ya maneno ya juu, wala si juu ya maneno yaliyo duniani.

Tito 2:11, 12

Kwa sababu neema ya Mungu inayoleta wokovu kwa watu wote, imeonekana, ikitufundisha sisi kukataa ubaya na tamaa za dunia, na kuishi na kiasi kwa haki, na utawa, katika ulimwengu wa sasa.

2 Timoteo 4:10

Maana Dema aliniacha, akiwa amependa dunia hii ya sasa, na alikwenda hata Tesalonika; Kreske kwa Galatia, Tito amekwenda Dalmatia.

1 Yoane 2:15, 16

Musipende dunia, wala maneno katika dunia. Mutu akipenda dunia, mapendo ya Baba si ndani yake. Maana kila kitu kilicho katika dunia, na tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitoki kwa Baba lakini vinatoka kwa dunia.

**Yoane 3:3**
Yesu akajibu, akamwambia: Kweli, kweli ninakuambia, Ila mutu azaliwe mara ya pili hawezi kuona ufalme wa Mungu.

**Ezekieli 36:26**
Nitawapa ninyi moyo mupya vilevile, nami nitatia roho mpya ndani yenu, na nitaondosha moyo wa jiwe toka mwili wenu, na nitawapa ninyi moyo wa mwili.

**2 Wakorinto 5:17**
Hivi kama mutu akiwa ndani ya Kristo, yeye ni kiumbe kipya; maneno ya zamani yamepita; tazama, maneno yote yamekuwa mapya.

**1 Yoane 2:29**
Kama mukijua ya kuwa yeye ni mwenye haki, jueni ya kuwa kila mutu anayetenda haki amezaliwa naye.

**1 Petro 1:23**
Kwa kuwa mumezaliwa tena, si kwa mbegu inayoharibika, lakini kwa ile isyoharibika, kwa Neno la Mungu lenye uzima linalodumu hata milele.

**1 Yoane 5:18**
Tunajua ya kuwa kila mutu aliyezaliwa na Mungu hatendi zambi; lakini yeye aliyezaliwa na Mungu anajilinda mwenyewe, wala yule mwovu hamugusi.

Wagalatia 5:24

Nao walio watu wa Kristo wamesulibisha mwili pamoja na mawazo mabaya na tamaa mbaya.

Wakolosayi 3:1

Basi mukiwa mumefufuliwa pamoja na Kristo, tafuteni maneno yaliyo juu, pahali Kristo yuko, akiketi mukono wa kuume wa Mungu.

1 Petro 2:24

Yeye mwenyewe alichukua zambi zetu katika mwili wake juu ya muti, hata sisi, tukiwa wafu kwa maneno ya zambi, tuwe hai kwa maneno ya haki; na kwa kupigwa kwake muliponyeshwa.

Waroma 6:2, 11

Hapana, hata kidogo. Sisi tuliokufia zambi, namna gani tutakaa ndani yake tena? . . . Hivyo ninyi mujihesabu wenyewe kuwa wafu kwa zambi, lakini walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu.

Waefeso 2:1, 6

Nanyi mulikuwa wafu kwa sababu ya makosa yenu na zambi zenu . . . na alitufufua pamoja naye na kutukalisha pamoja naye katika pahali pa mbingu, katika Kristo Yesu.

Yoane 3:36

Anayeamini Mwana ana uzima wa milele; na asiyetii Mwana hataona uzima, lakini gazabu ya Mungu inaikaa juu yake.

Waroma 6:23

Kwa maana mushahara wa zambi ni mauti, lakini zawadi ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana yetu.

Yoane 17:3

Na huu ni uzima wa milele, wakujue wewe, Mungu pekee wa kweli, na Yesu Kristo, uliyemutuma.

Yoane 3:14, 15

Na kama Musa alivyonyanyua nyoka jangwani, vivyo hivyo sharti Mwana wa watu anyanyuliwe, ili kila mutu akimwamini asipotee, lakini awe na uzima wa milele.

Yoane 5:24

Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Yeye anayesikia neno langu na kumwamini yeye aliyenituma ana uzima wa milele; hafiki kwa hukumu, lakini amepita kutoka mauti kuingia uzima.

Wagalatia 6:8

Maana yeye anayepanda kwa mwili wake mwenyewe, kwa mwili atavuna uharibifu; lakini yeye anayepanda kwa Roho, kwa Roho atavuna uzima wa milele.

**Wagalatia 4:6**
Lakini kwa sababu ninyi ni wana, Mungu alituma Roho ya Mwana wake katika mioyo yetu, anayelia: Aba, Baba.

**Yoane 14:21**
Aliye na amri zangu, na kuzitii, yeye ndiye mwenye kunipenda; naye anayenipenda atapendwa na Baba yangu, nami nitamupenda na kujionyesha mwenyewe kwake.

**Isaya 32:17**
Na kazi ya haki itakuwa salama; na mwisho wa haki, utulivu na tumaini kwa milele.

**1 Yoane 3:18, 19**
Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi lakini kwa matendo na kweli. Kwa hivi tutafahamu ya kwamba tuko wa kweli, nasi tutatuliza mioyo yetu mbele yake.

**1 Yoane 4:13**
Kwa hivi tunafahamu ya kuwa tunakaa ndani yake, naye ndani yetu, kwa kuwa ametugawia Roho yake.

**Waroma 8:16**
Roho mwenyewe anashuhudu pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu.

**Isaya 12:3**

Basi, kwa furaha mutateka maji katika visima vya wokovu.

**Yoane 15:11**

Maneno haya nimewaambia ninyi, kusudi furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe.

**Wagalatia 2:20**

Nimesulibiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai; wala si mimi, lakini Kristo ni hai ndani yangu; na uzima nilio nao sasa katika mwili, ni uzima wa imani iliyo ya Mwana wa Mungu aliyenipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.

**Zaburi 16:11**

Utanionyeshea njia ya uzima; Mbele ya uso wako ni furaha tele; Kwa mukono wako wa kuume ni mambo ya kupendeza kwa milele.

**Yoane 17:13**

Na sasa ninakuja kwako; na maneno haya ninayasema katika dunia, wawe na furaha yangu kutimizwa ndani yao.

**Waroma 14:17**

Kwa maana ufalme wa Mungu si kula na kunwya, lakini haki, na salama, na furaha katika Roho Mutakatifu.

Kwa sababu si wenye kusikia sheria walio wenye haki mbele ya Mungu, lakini wale wanaotenda sheria watakaohesabiwa haki. — Waroma 2:13

Hamujui ya kuwa kwake yeye munayejitoa wenyewe, kuwa watumwa wake wa kuti, mumekuwa watumwa wake munayemutii; ikiwa watumwa wa zambi hata kufa, ao ikiwa watumwa wa kutii hata haki? — Waroma 6:16

Na kuwalipa ninyi munaoteswa pumziko pamoja na sisi, wakati wa ufunuo wa Bwana Yesu kutoka mbingu pamoja na malaika za uwezo wake, katika moto wa kuwaka akiwalipa kisasi wao wasiojua Mungu, na wao wasiotii Habari Njema ya Bwana wetu Yesu Kristo; watakaoazibiwa kwa uharibifu wa milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake.

— 2 Watesalonika 1:7-9

Angalieni, ninaweka mbele yenu leo baraka na laana; baraka kama mutakaposikiliza maagizo ya BWANA Mungu wenu niliyowaagiza ninyi leo: na laana, kama musiposikiliza maagizo ya BWANA Mungu wenu . . .

—Kumbukumbu la Torati 11:26-28a

Matayo 10:32, 33

Basi kila mutu anayenikiri mbele ya watu, nitamukiri vilevile mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. Lakini kila mutu atakayenikana mbele ya watu, nitamukana vilevile mbele ya Baba yangu aliye mbinguni.

1 Yoane 2:23

Kila mutu anayekana Mwana hana Baba; anayekiri Mwana ana Baba vilevile.

Luka 9:26

Sababu kila mutu atakayeona haya juu yangu na juu ya maneno yangu, Mwana wa wau ataona haya juu ya mutu huyu siku ile atakapokuja katika utukufu wake, na wa Baba yake, na wa malaika watakatifu.

Wafilipi 2:11

Na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.

Waroma 10:9, 10

Kwa sababu kama ukikiri kwa kinywa chako ya kuwa Yesu ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimufufua toka wafu, utaokolewa: kwa maana kwa moyo mutu anaamini hata kupata haki; na kwa kinywa anakiri hata kupata wokovu.

Shetani asipate nafasi ya kutushinda; kwa sababu sisi hatukosi kujua hila zake.
—2 Wakorinto 2:11

Muwe na kiasi na kuangalia; adui yenu Shetani, kama simba ya kunguruma anazungukazunguka akitafua mutu amumeze.
—1 Petro 5:8

Vaeni silaha zote za Mungu, mupate kuweza kusimama juu ya hila za Shetani. —Waefeso 6:11

Kisha Yesu aliongozwa na Roho jangwani ajaribiwe na Shetani. . . . Ndipo Yesu alimwambia: Kwenda zako, Shetani; kwa sababu imeandikwa, Uabudu Bwana Mungu wako, umutumikie yeye peke yake. Kisha Shetani akamwacha; na tazama, malaika wakakuja wakamutumikia.
Matayo 4:1, 10, 11

Kuja kwa yule mwenye uasi ni kwa mufano wa kutenda kwa Shetani na uwezo wote, na alama na maajabu ya uwongo.
—2 Watesalonika 2:9

Uwafungulie macho yao, wageuke toka giza waingie nuru, watoke katika nguvu za Shetani na kufikia Mungu, ili wapate kusamehe kwa zambia zao, na uriti pamoja nao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu.
—Matendo 26:18

Yeye anayetenda zambi ni wa Shetani; kwa kuwa Shetani anatenda zambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alionekana, ili avunje kazi za Shetani. —I Yoane 3:8

Maana silaha za vita yetu si za mwili, lakini zina uwezo katika Mungu kuangusha maboma ya vita. —2 Wakorinto 10:4

Yakoba 4:7, 8a

Basi mutii Mungu, mushindane na Shetani, naye atawakimbia ninyi. Karibieni Mungu, naye atawakaribia ninyi.

Waebrania 2:14

Basi, kwa sababu watoto wameshiriki damu na mwili, yeye mwenyewe vivyo hivyo alishiriki kama wao, hata kwa njia ya kufa apate kuharibu yeye aliyekuwa na nguvu za kufa, ndiye Shetani.

2 Watesalonika 2:8

Wakati ule mwenye uasi atafunuliwa, ndiye Bwana Yesu atamwua kwa pumuzi ya kinywa chake, na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuja kwake.

Waroma 8:35, 37

Ni nani atakayetutenga na mapendo ya Kristo? Mateso, ao taabu, ao ufukuzo, ao njaa, ao utupu, ao hatari, ao upanga? . . . Lakini katika mambo haya yote, tunashinda na zaidi ya kushinda, kwa njia ya mwenye kutupenda.

**1 Yoane 4:20**

Kama mutu akisema: Ninapenda Mungu, naye anachukia ndugu yake, ni muwongo; kwa maana asiyependa ndugu yake aliyemwona, hawezi kupenda Mungu asiyemwona.

**Wagalatia 5:22, 23a**

Lakini matunda ya Roho ni mapendo, furaha, salama, uvumilivu, neema, wema, uaminifu, upole, ujizuiza . . .

**Yoane 13:35**

Hivi watu wote watajua ya kama ninyi wanafunzi wangu, kama ninyi mukiwa na mapendo ninyi kwa ninyi.

**Yoane 21:16**

Tena akamwambia mara ya pili: Simoni, mwana wa Yona, unanipenda? Akamwambia: Ndiyo, Bwana, unajua ya kama ninakupenda. Akamwambia: Chunga kondoo zangu.

**1 Wakorinto 13:1**

Kama nikisema na lugha za watu na za malaika, lakini sina mapendo, nimekuwa kama shaba inayolia, ao upatu wa kuvuma.

**1 Yoane 3:14**

Sisi tunajua ya kuwa tumepita toka mauti kuingia uzima, kwa maana tunapenda ndugu. Yeye asiyependa anakaa katika mauti.

Naye wakati alipofufuka asubui, siku ya kwanza ya juma, alionekana kwanza kwa Maria Magdalene kwake aliyemutokeza pepo saba. —Marko 16:9

Aliyetolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tuhesabiwe haki. —Waroma 4:25

Na nyuma ya siku nane wanafunzi wake walikuwa ndani tena, na Tomasi pamoja nao. Yesu akakuja, milango imefungwa, akasimama katikati, akasema: Salama kwenu. Basi akamwambia Tomasi: Leta hapa kidole chako, na tazama mikono yangu. Na leta hapa mukono wako uutie katika mbavu zangu; usiwe asiyeamini, lakini mwenye kuamini. Tomasi akajibu, akamwambia: Bwana yangu, na Mungu wangu.

—Yoane 20:26-28

Na sisi tuko washuhuda wa maneno yote aliyotenda katika inchi ya Wayuda, na katika Yerusalema; ndiye walimwua, wakamutundika mutini. Huyu Mungu alimufufua siku ya tatu, akamufanya aonekane wazi, si kwa watu wote, lakini kwa washuhuda waliochaguliwa na Mungu mbele, ndiyo sisi, tuliokula na kunywa pamoja naye nyuma ya ufufuko wake toka wafu.

—Matendo 10:39-41

Matayo 16:21

Toka wakati ule Yesu akaanza kuonyesha wanafunzi wake ya Kwamba imemupase kwenda yerusalema, na kupata mateso mengi kwa wazee na wakubwa wa makuhani na waandishi na kuuawa, na kufufuliwa siku ya tatu.

Yoane 5:25, 28, 29

Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Saa inakuja, na iko sasa, wakati wafu watakaposikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wale wanaosikia watakuwa hai.. . . Musishangae kwa maneno haya; kwa sababu saa itakuja na watu wote walio katika makaburi watasikia sauti yake, nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuko wa uzima, na wale waliofanya mabaya, kwa ufufuko wa hukumu.

Waroma 6:3-5

Ao hamufahamu, sisi sote tuliobatizwa katika Yesu Kristo, tulibatizwa katika kufa kwake? Hivi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika kufa: hata kama Kristo alivyofufuka toka wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo tutembee katika upya wa uzima vilevile. Kwa maana kama tulivyoungwa pamoja naye katika mufano wa kufa kwake, tutakuwa katika mufano wa ufufuko wake vilevile.

Lakini kama yeye aliyewaita ninyi ni mutakatifu, ninyi vilevile muwe watakatifu katika mwenendo wenu wote. —1 Petro 1:15

Ya kwamba atatupa sisi, tukiokolewa toka mikono ya adui zetu, Tumwabudu pasipo woga, Katika utakatifu na katika haki mbele yake, siku zote za maisha yetu. —Luka 1:74, 75

Basi kwa kuwa tuna ahadi hizi, wapenzi, tujisafishe kwa uchafu wote wa mwili na wa roho, tukitimiza utakatifu katika woga wa Mungu. —2 Wakorinto 7:1

Kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua ninyi katika utakaso wa Roho, kwa kutii na kunyunyiziwa damu ya Yesu Kristo: Neema na salama ziongezwe kwenu. —1 Petro 1:2

Tukikiri zambi zetu yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote. —1 Yoane 1:9

Basi kama mutu anajisafisha na hawa, atakuwa chombo cha kupata heshima, ametakaswa, na kufaa kwa kazi ya Bwana, ametengenezwa kwa kila kazi njema. —2 Timoteo 2:21

**Waefeso 1:4**

Kama vile alivyotuchagua ndani yake mbele ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, na pasipo kilema mbele yake katika mapendo.

**Waebrania 13:12**

Kwa sababu hii Yesu vilevile aliteswa inje ya lango, kusudi atakase watu wake kwa damu yake mwenyewe.

**Isaya 35:8**

Na njia kubwa itakuwa kule, na njia, nayo itaitwa njia ya utakatifu; wachafu hawatapita katikati yake; lakini itakuwa kwa ajili ya wale: wasafiri, hata wapumbavu, hawatapotea katika njia ile.

**2 Petro 3:11**

Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitayeyushwa hivi, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mutakatifu na utawa.

**Matayo 3:11**

Kweli mimi ninawabatiza ninyi kwa maji hata toba; lakini yeye anayekuja nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, na sistahili hata kuchukua viatu vyake; yeye atawabatiza ninyi kwa Roho Mutakatifu na kwa moto.

**Matendo 13:52**

Na wanafunzi walijaa furaha na Roho Mutakatifu.

**Waroma 8:9**

Lakini ninyi si kwa mwili, lakini kwa roho, kama Roho ya Mungu akikaa ndani yenu. Lakini kama mutu ye yote asipokuwa na Roho ya Kristo huyu si mutu wake.

**Luka 11:13**

Kama ninyi mulio wabaya munajua kuwapa watoto wenu zawadi njema, si zaidi Baba yenu aliye katika mbingu atawapa wote wanaomwomba Roho Mutakatifu.

**Matendo 4:31**

Na wakati walipokwisha kuomba, pahali walipokusanyika palitikiswa, wote wakajaa Roho Mutakatifu, wakasema Neno la Mungu pasipo woga.

**Matendo 1:8a**

Lakini mutapokea nguvu wakati Roho Mutakatifu anapokuja juu yenu, nanyi mutakuwa washuhuda wangu . . .

**Ezekieli 36:27**

Na nitaweka roho yangu ndani yenu na kuwatembeza ninyi kwa sheria zangu, na mutachunga hukumu zangu na kuzifanya.

Zaburi 37:3

Utumainie BWANA na tenda wema; Ukae katika inchi, na kufuata uaminifu.

Ufunuo 21:4

Naye atapangusa kila chozi katika macho yao; wala mauti haitakuwa tena; wala maombolezo, wala kilio, wala uchungu hautakuwa tena; kwa maana maneno ya kwanza yamekwisha kupita.

1 Petro 4:12, 13

Wapenzi, musishangae kwa majaribu ya moto yaliyo katikati yenu, yanayowapata ninyi kwa kuwapima ninyi, kama kwamba ni kitu kigeni kinachowapata ninyi. Lakini kama munavyoshiriki katika mateso ya Kristo, furahini, ili kwa wakati wa ufunuo wa utukufu wake mufurahi kwa shangwe.

Maana mukono wangu umefanya vitu hivi vyote, na vitu hivi vyote vimekuwa, BWANA anasema, lakini nitaangalia mutu huyu: mutu aliye masikini, mwenye roho ya kupondeka, na anayetetemeka kwa ajili ya neno langu. — Isaya 66:2

BWANA ni karibu na wenye moyo wa kuvunjika, Na anaokoa wenye roho ya toba.

—Zaburi 34:18

Waebrania 2:18

Na kwa kuwa yeye mwenyewe aliteswa wakati alipojaribiwa, anaweza kusaidia wale wanaojaribiwa.

Waroma 8:28

Na tunaiua maneno yote yanafanya kazi pamoja kuwapatia mema wale wanaopenda Mungu, kwa wale walioitwa kwa kusudi lake.

1 Wakorinto 10:13

Jaribu halikuwapata ninyi ila lililo kwa watu wote; lakini Mungu ni mwaminifu, asiyewaacha ninyi kujaribiwa kuliko munavyoweza; lakini pamoja na lile jaribu atafanya njia ya kukimbia, ili muweze kulivumilia.

Waroma 16:20

Na Mungu wa salama ataponda Shetani chini ya miguu yenu kwa upesi.

Zaburi 34:19

Mateso ya mwenye haki ni mengi; Lakini BWANA anamuponyesha nayo yote.

Isaya 43:2

Wakati unapopita katikati ya maji nitakuwa pamoja nawe; na katikati ya mito, haitakugarikisha; wakati unapotembea katikati ya moto, hutaungua, wala ulimi wa moto hautakuchoma.

Ufunuo 3:21

Yeye anayeshinda, nitamupa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha ufalme, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha ufalme.

Ufunuo 3:5

Yeye anayeshinda atavikwa nguo nyeupe, wala sitaondosha jina lake katika kitabu cha uzima; nami nitakiri jina lake mbele ya Baba yangu, na mbele ya malaika zake.

Ufunuo 3:12

Yeye anayeshinda nitamufanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, naye hatatoka tena kabisa; nami nitaandika juu yake jina la Mungu wangu, na jina la muji wa Mungu wangu, Yerusalema mupya, utakaoshuka toka mbingu kwa Mungu wangu; na jina langu mwenyewe, lile jipya.

Ufunuo 21:7

Yeye anayeshinda atariti maneno haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwana wangu.

Ufunuo 2:7

Yeye aliye na sikio, asikie neno Roho analoyaambia makanisa; Yeye anayeshinda nitamupa kula matunda ya muti wa uzima ulio katika shamba la Mungu.

**Matayo 5:32**

Lakini mimi ninawaambia ninyi: Kila mutu anayeacha muke wake, isipokuwa kwa habari za uasherati anamufanya kuwa muzini; na kama mutu akimwoa yule aliyeachwa, anazini.

**Luka 16:18**

Kila mutu anayeacha muke wake na kuoa mwingine, anazini; naye anayeoa yeye aliyeachwa na mume wake, anazini.

**Waroma 7:2, 3**

Kwa sababu mwanamuke aliye na mume amefungwa na sheria kwa mume wake angali anapokuwa ni hai: lakini kama yule mume amekufa, amefunguliwa kwa sheria ya mume. Basi kama akiwa na mume mwingine, angali mume wake anapokuwa ni hai, ataitwa muzini; lakini kama mume wake amekufa, amekuwa huru kwa sheria; hata yeye si muzini hata akiwa na mume mwingine.

**1 Wakorinto 7:10, 11**

Nao waliokwisha kuoana, ninawaagiza, wala si mimi, lakini Bwana, Muke asiachane na mume wake. Lakini kama ikiwa ameachana naye, abaki pasipo mume, ao apatane na mume wake: na mume asiache muke wake.

Marko 8:38

Maana kila mutu anayesikia haya juu yangu na juu ya maneno yangu katika kizazi hiki cha uzini na zambi, Mwana wa watu atasikia haya juu yake wakati atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.

Matayo 24:30

Halafu alama ya Mwana wa watu itaonekana mbinguni; na mataifa yote ya dunia wataomboleza, nao wataona Mwana wa watu akikuja katika mawingu ya mbingu pamoja na uwezo na utukufu mukubwa.

Yoane 14:3

Na kama ninakwenda kuwatengenezea ninyi pahali, nitakuja tena, na nitawakaribisha ninyi kwangu; pahali ninapokaa mimi, mukae vilevile.

Matayo 24:27

Kwa maana kama umeme unavyokuja toka mashariki na unaonekana hata mangaribi; hivi kuja kwa Mwana wa watu kutakavyokuwa vile.

Yakobo 5:8

Nanyi vumilieni, mutie mioyo yenu nguvu, kwa sababu kuja kwake Bwana kunakaribia.

Tazama ninakuja kama mwizi. Heri yeye anayeangalia na kutunza mavazi yake, asiende wichi, watu wakaona haya yake.
—Ufunuo 16:15

Na wakati ule wataona Mwana wa watu akikuja katika wingu pamoja na uwezo na utukufu mukubwa. —Luka 21:27

Nanyi basi, muwe tayari, kwa sababu Mwana wa watu anakuja saa musipozania. —Luka 12:40

Wakasema: Ninyi watu wa Galilaya, kwa sababu gani mumesimama mukitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa toka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja namna hii sawasawa mulivyomwona akikwenda zake mbinguni. —Matendo 1:11

Wapenzi, sasa tuko wana wa Mungu wala haijaonekana bado tutakuwa namna gani; lakini tunajua wakati atakapoonekana tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo.
—1 Yoane 3:2

Kwani Mwana wa watu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake, na halafu atamupa kila mutu kwa kadiri ya matendo yake.
—Matayo 16:27

## NENO LA MUNGU

**Maana unabii wo wote haukuletwa kwa mapenzi ya mutu, lakini watu walisema yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mutakatifu. —2 Petro 1:21**

**Lakini Yesu akajibu, akawaambia: Munakosa kwa sababu hamujui maandiko wala uwezo wa Mungu. —Matayo 22:29**

**Musiongeze juu ya neno nililowaamuru ninyi, wala musilipunguze, mupate kushika amri za BWANA Mungu wenu nilizowaamuru ninyi. —Kumbukumbu la Torati 4:2**

**Nimeficha neno lako moyoni mwangu, Nisikukosee. —Zaburi 119:11**

**Kila andiko limepewa kwa maongozi ya Mungu, na linafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu juu ya makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa mafundisho katika haki. —2 Timoteo 3:16**

**Mbingu na dunia zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kabisa. —Luka 21:33**

**Neno lako ni taa kwa miguu yangu, Na nuru kwa nija yangu. —Zaburi 119:105**

Text from the Bible in revised Swahili, Congo by permission of the Bible Society of Dem. Rep. of Congo (Africa). The entire New Testament or Bible may be obtained from your church, religious bookstore, or the Bible Society.

Published in numerous languages by World Missionary Press as God supplies funds in answer to prayer. If you would like more copies for careful distribution, write in English to:

**World Missionary Press, Inc.**
**P.O. Box 120**
**New Paris, IN 46553-0120**

www.wmpress.org 3-15 95 Swahili, Congo (RDC) HFA